

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA**



Agosti 27, 2022

**MKUU WA MKOA WA NJOMBE MHE. ANTHONY MTAKA AMEFANYA ZIARA YA  
KIKAZI WILAYA YA LUDEWA**

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mheshimiwa Andrea Tsere leo Agosti 27, 2022 amempokea Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka aliyefanya ziara ya kikazi katika Wilaya ya Ludewa.

Mhe. Anthony Mtaka amekagua zoezi la sensa linaloendelea Wilaya ya Ludewa huku Wilaya hiyo ikiwa imefanikiwa kuwafikia wananchi wote wa Wilaya ya Ludewa na kuifanya Wilaya hiyo kufikia asilimia zaidi ya 98.

Aidha Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa amewapongeza makarani wote kwa uadilifu mkubwa wanaoendeleanao kwa kufuata maelekezo aliyoyatoa jana kuwahesabu wananchi kwenye kaya zao kwa kukaa nje na kupata taarifa zote za msingi.

Pamoja na mambo mengine Mhe. Anthony Mtaka ametembelea kaburi la Hayati **Horace Kolimba** lililopo Wilayani Ludewa katika Kata ya Masasi Kijiji cha Manda.

Ziara hiyo imehudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwemo Mbunge wa Jimbo la Ludewa Mhe. Joseph Kamonga, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratias pamoja na kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Ludewa.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Chrispin B. Kalinga'.

**Chrispin B. Kalinga**  
**Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini**  
**Halmashauri (W) Ludewa.**